

**MITAZAMO YA WALIMU KUHUSU TEKNOLOJIA YA
MAWASILIANO KATIKA UFUNZAJI NA UJIFUNZAJI WA
KISWAHILI KATIKA KAUNTI NDOGO YA KASIPUL, KENYA**


**BENSON ONYANGO OCHIENG
E55/CE/24223/2012**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA TAALUMA YA
ELIMU NA UFUNDISHAJI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

AGOSTI, 2017

UNGAMO

Utafiti huu ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine.

Sahihi:  Tarehe: 28/08/2017

Benson Onyango Ochieng

E55/CE/24223/2012

Tasnifu hii imewasilishwa ili kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

WASIMAMIZI:

Sahihi:  Tarehe: 28/8/17

Dkt. Hamisi Omar Babusa

Idara ya Mawasiliano ya Elimu na Teknolojia – Chuo kikuu cha Kenyatta.

Sahihi:  Tarehe: 29/08/2017

Dkt. Florence A. Miima

Idara ya Mawasiliano ya Elimu na Teknolojia – Chuo kikuu cha Kenyatta.

IKISIRI

Utafiti huu ulinua kuchunguza mitazamo ya walimu katika kushirikisha matumizi ya Teknolojia ya Mawasiliano katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili za Kaunti Ndogo ya Kasipul, Kaunti ya Homabay, Kenya. Utafiti wenyewe ulizingatia teknolojia mpya kama vile teknolojia za kompyuta pamoja na mtandao. Idadi iliyofanyiwa utafiti ilijumuisha walimu 52 wa Kiswahili, walimu wakuu 24 wa shule za upili na wanafunzi 2140. Utafiti huu ulichunguza misingi ya mitazamo ya walimu kuhusu ushirikishaji wa teknolojia ya mawasiliano katika ufundishaji wa Kiswahili katika kaunti ndogo ya Kasipul. Madhumuni ya utafiti huu ulikuwa; kutathmini mitazamo ya walimu kuhusu matumizi ya teknolojia ya mawasiliano katika ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili, kubainisha viwango vya walimu vya matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika ufundishaji wa Kiswahili na kuchunguza changamoto zinazowakumba walimu katika kuitumia teknolojia ya mawasiliano darasani. Kwa kuzingatia misingi ya nadharia ya Ubunaji, misingi ya mitazamo ya walimu kuhusu kushirikisha teknolojia katika ufundishaji wa Kiswahili ulitathminiwa. Muundo wa kimaelezo ulitumika katika utafiti huu. Vifaa ambavyo vilitumiwa katika utafiti huu ni hojaji, uchunzaji pamoja na mahojiano. Maswali yaliyotumiwa katika hojaji yalikuwa maswali wazi, maswali funge na maswali ya viwango. Walimu wakuu, walimu wa Kiswahili na wanafunzi walihojiwa ili kupambanua mitazamo yao katika ushirikishaji wa teknolojia ya mawasiliano katika ufundishaji wa Kiswahili. Data ilichanganuliwa kwa kutumia majedwali ya frikwenzi pamoja na vielelezo. Matokeo ya utafiti yalinuiwa kusababisha kuimarika kwa utekelezaji na ujumuishaji wa teknolojia ya mawasiliano katika somo la Kiswahili kwa kutambua changamoto za utekelezaji na ujumuishaji katika msingi wa mitazamo kuhusu matumizi ya teknolojia ya mawasiliano. Hali kadhalika, yalinuiwa kuimarisha mtaala wa Kiswahili ili uweze kukidhi zaidi mahitaji ya walimu na wanafunzi kwa kuwawezesha kukabili vizuizi pamoja na kuwa msingi wa utafiti zaidi. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa mitazamo ya walimu kuhusu teknolojia ya mawasiliano ilikuwa chanya. Kwa kiwango fulani, mitazamo ya walimu katika ufundishaji wa Kiswahili kwa kutumia teknolojia ya mawasiliano kuliathiriwa na vigezo kama umri, jinsia na kiwango cha kielimu. Kufuatia matokeo haya, ilipendekezwa kuwa walimu wa Kiswahili na hata wale walio kwenye vyuo mbalimbali wapewe mafunzo zaidi kuhusu matumizi ya teknolojia ya mawasiliano katika ufundishaji. Matokeo ya utafiti yananiwa kujaza pengo katika utoaji wa mafunzo ya Kiswahili na vile vile kuwasaidia wakuza mitaala kufanikisha zoezi la ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili.